

## Ridhaa ya kushiriki kwenye Utafiti

Umealikwa kushiriki kwenye uchunguzi wa kitafiti. Kabla haujakubali, ni lazima upewe muhtasari wa utafiti. Muhtasari huu utakuwa na taarifa muhimu zitakazokusaidia kuelewa sababu zitakazokufanya aidha ukubali kujinga au uchague kutokujiunga na utafiti.

Kabla ya kukubali, mpelelezi lazima akueleze kuhusu:

- (i) Sababu, mbinu na muda wa utafiti.
- (ii) Mbinu zozote ambazo ni za kimajaribio
- (iii) Hatari za msingi zionekanazo, masumbufo na faida za utafiti
- (iv) Uwezekano wowote wa matibabu au taratibu mbadala zenyne faida
- (v) Jinsi usiri utakavyodumshwa; na
- (vi) Nani wa kuwasiliana naye kwa maswali, malalamiko na majeraha

Ambapo itatakiwa, mpelelezi atalazimika kukwambia pia kuhusu:

- (i) Fidia zozote zilizopo au matibabu iwapo jeraha litatokea.
- (ii) Uwezekano wa hatari zisizoonekana.
- (iii) Mazingira ambayo mpelelezi atasimamisha ushiriki wako.
- (iv) Gharama zozote zitakazoongezeka kwako.
- (v) Kitakachotokea ukiamua kusitisha ushiriki.
- (vi) Lini utakapo ambiwa kuhusu uvumbuzi mpya ambao utaathiri utayari wako wa kushiriki.
- (vii) Idadi ya watu watakaokuwepo kwenye uchunguzi; na
- (viii) Jinsi utakavyohitajika kuidhinisha matumizi ya taarifa zako za matibabu kwa ajali ya utafiti

Ushiriki wako kwenye utafiti huu ni wa hiari, na hauta adhibiwa wala kupoteza faida kama ukikataa kushiriki au ukiamua kusitisha ushiriki. Kutia sahihi waraka huu inamanisha kuwa utafiti, ukijumlisha taarifa za hapo juu, zimeelezwa kwako kwa mdomo na kwamba umekubali kwa hiari kushiriki. Kama umekubali kushiriki, ni lazima ukabidhiwe nakala ya waraka huu iliyotiwa sahihi na muhtasari wa utafiti ulioandikwa kwa kiingereza.

### Maswali?

Kama una maswali yoyote, malalamiko, majeraha au jambo lolote kuhusu utafiti, unaweza wasiliana na mpelelezi kwa kutumia namba za simu zilizoainishwa kwenye muhtasari wa utafiti ulioandikwa. Kama unaswali kuhusu haki zako kama mshiriki au una maswali, malalamiko, majeraha au jambo ambalo unahisi huwezi jadili na mpelelezi, tafadhalii wasiliana na ofisi ya Bodi ya taasisi ya Ukaguzi kwa kutumia namba ya simu au anwani ya barua pepe iliyopo kwenye muhtasari wa utafiti.

---

Jina la Mshiriki

---

Sahihi ya mshiriki

---

Tarehe

Ninaidhinisha ya kwamba nilikuwepo kama mkalimani kwa kipindi chote cha mchakato wa ridhaa kwa ajili ya utafiti huu. Ninaidhinisha ya kwamba ninastahili na ujuzi wote unaohitajika kutoa tafsiri katika Kiingereza na lugha ya mwamali. Kwa kutia sahihi katika fomu hii, ninaidhinisha ya kwamba nimetoa tafsiri yote na iliyokamili ya mazungumzo katika ya mtafiti kupokea ridhaa na mwamali, kwa kadiri ya uwezo wangu.

---

Jina la Mkalimani

---

Sahihi ya Mkalimani

---

Tarehe